## DAWA ZA KISASA ZA KUFUBAISHA VVU ZINAZOTUMIKA TANZANIA

# DAWA ZA KUFUBAISHA VVU (ART) UJAUZITO NA AFYA YA WANAWAKE

**Kila mtu mwenye maambukizi ya VVU anatakiwa kupata tiba ya kufubaisha VVU inayojulikana kama Dawa za Kurefusha Maisha, Dawa za Kufubaisha VVU (ART) au ARV.**

NOVEMBA 2020



# JE, WATU WENYE VVU WANAWEZA KUPATA WATOTO WASIO NA VVU?




## NDIYO!

Dawa za kufubaisha makali ya VVU (ART) hulinda mtoto wako dhidi ya VVU wakati wa Ujauzito, Kuzaliwa na wakati wa Kunyonyesha.

Zungumza na Muuguzi au Daktari wako juu ya hili.

# JE MATIBABU NI YALEYALE KWA WANAWAKE WAJAWAZITO KAMA YALIVYO KWA WATU WENGINE WENYE MAAMBUKIZI YA VVU?

**Miongozo ya nchini Tanzania sasa inapendekeza matumizi ya dawa za kufubaisha VVU (ART) kwa kila mtu aliye na VVU pasipo kujali idadi ya CD4 au uwingi wa virusi katika damu.**



## Hii hujumuisha wanawake wajawazito na wanawake wanaotaka kubeba ujauzito.

**Kuna mambo machache ya ziada ambayo wanawake wanapaswa kuzingatia pindi wanapoanza kutumia dawa za kufubaisha VVU (ART) au wakati wakiwa wanatumia dawa za kufubaisha VVU (ART).**

**Tunaelezea mambo yote hayo ndani ya Kijitabu hiki.**

# MCHANGANYIKO WA DAWA ZA KUPUNGUZA MAKALI YA VVU (ARVS) NCHINI TANZANIA

Tiba ya kipaumbele ya kufubaisha VVU hujumuisha dawa tatu za kupunguza makali ya VVU (ARVs) ndani ya kidonge kimoja-ambacho huitwa mchanganyiko wa dozi ya kudumu.

Tiba ya kipaumbele ya Kufubaisha VVU nchini Tanzania hujumuisha: tenofovir, lamivudine na dolutegravir. Mchanganyiko huu wakati mwingine huitwa TLD.

Mchanganyiko wa zamani wa Tiba ya kipaumbele ya Kufubaisha VVU ulitokana na kidonge kiitwacho efavirenz.



# DOLUTEGRAVIR NA UJAUZITO



**Kuna kiwango kikubwa kiasi kuliko kawaida cha kupata dosari au matatizo katika mshipa wa neva kwa watoto ambao mama zao hubeba ujauzito katika kipindi ambacho wanatumia dolutegravir.**

**Lakini kuanza kutumia Dolutegravir wiki 6 au zaidi tangu kubeba ujauzito huwaepusha na hatari hii.**

# JE, MATATIZO YA MSHIPA WA NEVA NI NINI?

**Mshipa wa neva kwa watoto walioko tumboni ndio kiungo ambacho hugeuka na kuwa ubongo, uti wa mgongo, na fuvu.**

**Mshipa wa neva hujifunga ndani ya siku 28 za ujauzito-kipindi ambacho wanawake wengi wanakuwa hawajui kama ni wajawazito.**

**Ikiwa mshipa wa neva hautojifunga barabara, basi mtoto atapata matatizo ya mshipa wa neva.**






**Matatizo ya mshipa wa neva hutofautiana, kuanzia yale madogo ambayo yanaweza kutibika kirahisi hadi yale makubwa ambayo huweza kusababisha ulemavu wa kudumu au hata kifo.**

**Hivyo basi, hatari hii inatiliwa maanani sana na idara ya afya, watumishi wa afya pamoja na wagonjwa.**

# JE, WANAWAKE WENYE MAAMBUKIZI YA VVU WANAWEZA KUTUMIA DOLUTEGRAVIR KWA USALAMA?

# NDIYO!*

**Lakini kwa kuzingatia mambo machache zaidi.**

*** Wanawake wote wenye maambukizi ya VVU wanapaswa kufahamishwa na watumishi wa afya juu ya machaguo yao ili waweze kuchagua mchanganyiko sahihi wa dawa za kupunguza makali ya VVU.**

# JE, ITAKUWAJE NIKIWA TAYARI NINA UJAUZITO?

**Ikiwa tayari ni mjamzito na unatumia dawa ya kufabaisha VVU yenye Dolutegravir, utashauriwa kuendelea kutumia dawa hiyo.**

# JE, VIPI KAMA SIHITAJI KUBEBA UJAUZITO?

**Iwapo hauhitaji kubeba ujauzito na unatumia njia thabiti za uzazi wa mpango basi utashauriwa kutumia mchanganyiko wenye dolutegravir.**

**Njia thabiti za uzazi wa mpango ni njia za kisasa za kuzuia ujauzito: Matumizi ya kondomu, vidonge vya kuzuia mimba, vipandikizi, na IUCD.**

# JE, ITAKUWAJE IKIWA NAHITAJI KUBEBA UJAUZITO?

**Ikiwa unapanga kubeba ujauzito unapaswa kupewa taarifa zote kuhusiana na mchanganyiko wa vidonge vya kufubaisha VVU wenye Dolutegravir na ule wenye efavirenz.**

**Hii ni pamoja na hatari ya kasoro za mshipa wa neva. Hakikisha umepewa taarifa zote unazozihitaji. Daktari wako lazima ahakikishe kuwa umefanya maamuzi sahihi. Taarifa hizi lazima ziingizwe kwenye chati au faili lako.**

# HAKIKISHA UNAFURAHIA UAMUZI WAKO


## Hii ni muhimu sana!

**Ni muhimu pia kufahamu kwamba ikiwa utachukua maamuzi ya kupata mtoto na unatumia dawa za kufubaisha VVU zenye Dolutegravir huku ukiwa na wasiwasi juu ya uwezekano wa mtoto kupata dosari katika mshipa wa neva unaweza kubadilisha dawa na ukaanza kutumia dawa za efavirenz.**

**Au, ukiamua kutumia efavirenz katika kipindi cha kubeba ujauzito, unaweza kubadili na kuanza kutumia dolutegravir hapo badae.**

**Unaweza kubadili dawa ikiwa kiasi cha VVU kwenye damu kimepungua na kufikia hatua ya kutoonekana.**






# JIHADHARI!


**Afya yako mwenyewe pamoja na matibabu yako ya kufubaisha VVU ni vitu vya kuzingatia sana ili kuhakikisha kuwa unapata mtoto mwenye afya.**

# FAHAMU MACHAGUO YAKO

Hakikisha unafahamu machaguo yako- Ikiwa ni pamoja na kupata taarifa katika jarida kama hili.

Hakikisha kuwa watoa huduma wa afya wanajadili na wewe juu ya machaguo yako na wanaheshimu maamuzi yako.






**Fahamu zaidi juu ya matibabu na App yetu ya bure kwa kutembelea:**

**www.modernartforsouthafrica.co.za**

**@modernart4sa**

i-base

AFROCAB

PEPFAR

CRS CATHOLIC RELIEF SERVICES

CLINTON HEALTH ACCESS INITIATIVE

